# ZANA ZA MAFUNDISHO KWA FAMILIA

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Shepherds Global Classroom ipo kwa ajili ya kuujenga mwili wa Kristo kwa kutoa mtaala kwa ajili ya kuwaendeleza viongozi wa Kikristo duniani kote. Tunalenga kuongeza programu za mafunzo ya asili kwa kuweka chombo cha mtaala wa kozi 20 mikononi mwa viongozi wa kiroho wanaotoa mafunzo katika kila nchi duniani.

Kitabu hiki kinapatikana bure kwa njia ya kupakua kutoka katika https://www.shepherdsglobal.org/courses

Hakimiliki © 2023 Shepherds Global Classroom
Toleo la kwanza.

Haki zote zimehifadhiwa.

**Maswali na Majibu kwa Watoto Wadogo**

Mwandishi: Johnathan Arnold
Kutoka kitabu cha Johnathan Arnold, *Holy Joys Kids' Catechism*, 2022. Kwa toleo la katekisimu la kuchapishwa lenye michoro mizuri, tembelea https://holyjoys.org/shop. Imetumika kwa idhini.

**Maswali na Majibu kwa Watoto**

Waandishi: Dr. Matt Friedman na Dr. Ray Easley
Kutoka Dr. Matt Friedeman's book, *Discipleship in the Home*, (Wilmore: Francis Asbury Society, 2010), pp. 125-143. Imetumika kwa idhini, ikiwa imefupishwa kidogo kutoka maswali 126 hadi 116, pamoja na mabadiliko madogo

**Kanuni kutoka Mithali**

Mwandishi: Dr. Stephen K. Gibson

**Taarifa kuhusu vibali:**

Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa na kutawanywa bure kikiwa kimechapishwa na katika mifumo ya kidigitali chini ya miongozo ifuatayo: (1) Maudhui yaliyoko kwenye kitabu hiki hayawezi kubadilishwa kwa namna yeyote ile; (2) Nakala zinazopatikana haziwezi zikauzwa kwa ajili ya kupata faida; (3) Taasisi za elimu zina uhuru wa kutumia na kukinakili kitabu hiki, hata kama wanalipisha ada za masomo ya ziada; na (4) Kitabu hiki hakiwezi kufanyiwa tafsiri pasipokuwepo na kibali na usimamizi wa Shepherds Global Classroom.

# Yaliyomo


Imani ya Mitume ........................................ 4

Sala ya Bwana ........................................ 4

Kwa wazazi: Zana ya 1 & 2 ........................................ 5

Maswali na Majibu kwa Watoto Wadogo ........................................ 7

Maswali na Majibu kwa Watoto ........................................ 13

Kwa Wazazi: Zana ya 3 ........................................ 25

Kanuni kutoka Mithali ........................................ 27

# Imani ya Mitume

Namwamini Mungu Baba mwenyezi,
muumba mbingu na nchi:
Na Yesu Kristo Mwana wake pekee, Bwana wetu.
aliyechukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu,
akazaliwa na bikira Mariamu,
akateswa zamani za Pontio Pilato,
akasulubiwa, akafa, akazikwa,
akashuka mahali pa wafu;
siku ya tatu akafufuka,
akapaa mbinguni,
ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi,
kutoka huko atakuja
kuwahukumu walio hai na watu wafu.

Namwamini Roho Mtakatifu;
na kanisa takatifu ya Waamini wote;
na ushirika wa watakatifu;
na ondoleo la dhambi;
na kiyama ya mwili;
na uzima wa milele. Amina.

# Sala ya Bwana

Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe,
Ufalme wako uje,
Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.
Utupe leo riziki yetu.
Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.
Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.
Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

- Mathayo 6:9-13

# Kwa wazazi: Zana ya 1 & 2

## Kufundisha kwa maswali na Majibu

Kuuliza maswali na kutoa majibu mafupi na rahisi ni mbinu bora ya kufundisha ambayo imetumika kwa karne nyingi.

Maswali na majibu yaliyomo katika kitabu hiki yanaanzisha mafundisho ya msingi ya imani ya Kikristo.

**Zana ya 1** inafaa kwa kufundisha watoto wadogo sana. Inatoa msingi imara wa mafundisho ya baadaye wanapokua

**Zana ya 2** inafaa kufundisha watoto wakubwa kidogo na waongofu wapya. Majibu yanayotolewa ni maelezo mafupi ambayo yanatoa fursa ya majadiliano na kujifunza zaidi. Mafundisho haya ni kama ramani ya nyumba: si kamilifu yenyewe, lakini hutoa muundo wa kujenga maelezo ya kina ya imani ya Kikristo.

## Jinsi ya Kutumia Zana Hizi kama Familia

Ili kutumia vizuri rasilimali hizi, majibu ya kila swali yanapaswa kukaririwa kwa usahihi kama yalivyoandikwa. Majibu yasifupishwe wala kubadilishwa maneno. Badala yake, maneno halisi yasomwe na kukaririwa. Kukariri maneno halisi husaidia katika kumbukumbu ya muda mrefu na huwasaidia wanafunzi kuwa makini na sahihi.

Tenga dakika 10 kila siku kupitia maswali na majibu kutoka kitabu hiki. Baadhi ya familia wanaona kuwa wakati wa kula, ambapo kila mtu yupo, ndio muda mzuri wa kujifunza.

Ni kiongozi tu wa kipindi cha mafundisho ndiye anayepaswa kuwa na kitabu mkononi. Kiongozi atasoma swali kisha ataje jibu huku wengine wakisikiliza, halafu wote waseme pamoja.

Rudia kusoma swali na jibu, ukimfanya mtoto mdogo afuate. Mtu mzima aendelee kurudia swali. Polepole (kwa siku kadhaa), mtu mzima aache kusema jibu, na mtoto aseme maneno peke yake anapokariri vizuri. Mtu mzima auliza, mtoto ajibu—hii ndiyo kiini cha kujifunza kwa njia ya maswali na majibu.

### Maelekezo ya Ziada kwa Zana ya 2

Ongeza swali jipya kila mara kila mtu anapokaribia kukariri jibu la awali kwa usahihi.

Endelea kushuka kwenye orodha, ukiendelea kupitia, kupitia, na kupitia tena, huku ukiongeza maswali polepole pindi maneno mengi ya swali na jibu la mwisho yanapokumbukwa.

Wakati sehemu nzima ya maswali inaweza kusemwa pamoja, rudia sehemu hiyo yote mara moja kwa wiki ili kusaidia majibu kuhamia kutoka kwenye kumbukumbu ya muda mfupi hadi ya muda mrefu.

Ongeza mambo mapya polepole na endelea kurudia—njia hizi mbili zitaleta matokeo ya kushangaza miongoni mwa wanafunzi wanaotumia muda kidogo tu wakifuata uongozi wa mwalimu, rafiki, au mzazi mwenye moyo wa kujali. Vifanye vipindi vya kujifunza viwe vya kufurahisha na sherehekea mafanikio ya mwanafunzi.

Unaweza kujumuisha maswali na majibu haya kama sehemu ya ibada ya kila siku ya kifamilia. Unaweza kuyatumia katika ibada za watoto kanisani, kwa mashindano kati ya makundi ya watoto. Pia unaweza kuandaa maelezo na mifano ya ziada kusaidia wanafunzi kuelewa vizuri zaidi.

## Mpango Mmoja wa Ibada ya Familia

Kuna njia nyingi za kufanya ibada ya familia kwa pamoja. Huu hapa ni mpangilio mmoja wa ibada ya familia ambapo zana hizi zinaweza kutumika:

1. Imba wimbo wa tenzi au sifa.
2. Sema **Imani ya Mitume**.
3. Fanya mazoezi ya kukariri sehemu ya **maswali na majibu** ya imani.
4. Soma sura au kifungu kutoka katika Biblia. (Anza kwa kusoma Injili za Mathayo, Marko, Luka, na Yohana.)
5. Ombeni, baada ya kuuliza mahitaji ya maombi. (Unaweza kuuliza: “Tunawezaje kukuombea wewe?” na “Tunawezaje kuwaombea wengine?”)
6. Hitimisha kwa **Sala ya Bwana**.

# Zana ya 1
# Maswali na Majibu kwa Watoto Wadogo

## Maswali ya Kwanza

1. Nani anakupenda zaidi ya Mama na Baba?

   Jibu: Mungu

2. Kwa nini Mungu alikuumba?

   Jibu: Ili niwe na furaha

3. Unawezaje kuwa na furaha?

   Jibu: Kwa kumpenda Mungu

4. Je, kuna kitu kingine kinachoweza kukufanya uwe na furaha milele?

   Jibu: Hapana

## Mungu

5. Kuna miungu mingapi?

   Jibu: Mungu mmoja

6. Kuna nafsi ngapi ndani ya Mungu?

   Jibu: Nafsi tatu

7. Nafsi ya kwanza katika Mungu ni nani?

   Jibu: Baba

8. Nafsi ya pili katika Mungu ni nani?

   Jibu: Mwana

9. Nafsi ya tatu katika Mungu ni nani?

   Jibu: Roho Mtakatifu

## Uumbaji

10. Nani aliumba vitu vyote?

    Jibu: Mungu Baba

11. Mungu aliumba vitu vyote kwa kupitia nani?

    Jibu: Mwana na Roho

12. Kwa nini Mungu anaweza kuumba vitu vyote?

    Jibu: Kwa sababu yeye ni Mwenye Nguvu Zote

## Binadamu

13. Mungu alikuumba vipi?

    Jibu: Kwa mfano wake

14. Hili linakufariji vipi?

    Jibu: Mimi ni wa maana mbele za Mungu.

15. Kwa kuwa kila mtu ameumbwa kwa mfano wa Mungu, tunapaswa kuwatendeaje?

    Jibu: Kwa upole na heshima

## Dhambi

16. Ni nani waliokuwa mwanamume na mwanamke wa kwanza?

    Jibu: Adamu na Hawa

17. Adamu na Hawa walifanya nini?

    Jibu: Walitenda dhambi

18. Dhambi ni nini?

    Jibu: Kutomtii Mungu

19. Adhabu ya dhambi ni nini?

    Jibu: Kifo

## Yesu Kufanyika Mwili (Umwilisho)

20. Mungu alimtuma nani atuokoe kutoka dhambini na mauti?

    Jibu: Mwanawe wa pekee

21. Mwana wa Mungu ni nani?

    Jibu: Yesu Kristo

22. Mama yake Yesu alikuwa nani?

    Jibu: Bikira Mariamu

23. Nani alimpa Mariamu mtoto Yesu?

    Jibu: Roho Mtakatifu

## Upatanisho

24. Yesu alikufa vipi?

    Jibu: Alisulubiwa

25. Kwa nini Yesu alikufa?

    Jibu: Kwa ajili ya dhambi zetu

26. Nini kilitokea siku ya tatu?

    Jibu: Alifufuka tena

27. Kwa sababu Yesu alikufa na kufufuka, tunaamini nini?

    Jibu: Yeye ni Bwana

## Wokovu

28. Yesu alikwenda wapi?

    Jibu: Kwa Baba yake mbinguni

29. Yesu anafanya nini sasa?

    Jibu: Anatawala kama Mfalme

30. Kwa nini Yesu anarudi tena?

    Jibu: Kuwahukumu watu wote

31. Lazima ufanye nini ili uokoke?

    Jibu: Nimwamini Yesu

32. Utafanya nini ukitenda dhambi?

    Jibu: Niseme pole kwa Mungu

## Roho Mtakatifu na Kanisa

33. Mungu alimtuma nani mwingine atuokoe?

    Jibu: Roho Mtakatifu

34. Roho Mtakatifu anakufanyia nini?

    Jibu: Ananisaidia

35. Roho Mtakatifu anakusaidiaje?

    Jibu: Kupitia Kanisa

36. Kanisa ni nini?

    Jibu: Familia ya Mungu

37. Unaunganishwaje na Kanisa?

    Jibu: Kupitia ubatizo

**Faraja**

38. Je, unapaswa kuwa na hofu?

    Jibu: Hapana

39. Kwa nini huhitaji kuwa na hofu?

    Jibu: Mungu yupo pamoja nami

40. Je, unaweza kumuona Mungu?

    Jibu: Hapana

41. Je, Mungu anakuuona wewe?

    Jibu: Ndiyo

**Utakaso**

42. Mungu anataka uwe kama nani?

    Jibu: Yesu

43. Mapenzi ya Mungu kwako ni nini katika amri nne za kwanza?

    Jibu: Kumpenda Mungu

44. Mapenzi ya Mungu kwako ni nini katika amri sita za mwisho?

    Jibu: Kumpenda jirani yangu

45. Mungu anataka umtii nani?

    Jibu: Mama na Baba

46. Maombi ni nini?

    Jibu: Kuongea na Mungu

47. Yesu alitufundisha kuomba nini?

    Jibu: Sala ya Bwana

48. Mungu anazungumzaje nawe?

    Jibu: Kupitia Biblia

49. Biblia ni nini?

    Jibu: Neno la Mungu

## Mambo ya Mwisho

50. Mungu anafanya upya nini?

    Jibu: Vitu vyote

51. Mungu atafufua nini kutoka kwa wafu?

    Jibu: Miili yetu

52. Tunafurahia nini sasa na tunatarajia kufurahia milele?

    Jibu: Uzima wa milele

## Amri Kumi za Mungu (Kwa Lugha Rahisi)

Mimi ni Bwana Mungu wako, niliyekuokoa.

1. Usiwe na miungu mingine ila Mimi.
2. Usijifanyie sanamu ya kuabudu.
3. Usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako.
4. Ikumbuke siku ya Sabato uitakase.
5. Waheshimu baba yako na mama yako.
6. Usiue.
7. Usizini.
8. Usiibe.
9. Usiseme uongo.
10. Usitamani mali ya mtu mwingine.

# Zana ya 2
# Maswali na Majibu kwa Watoto

## Maswali kuhusu Biblia

1. Ni wapi tunajifunza jinsi ya kumpenda na kumtii Mungu?

   Jibu: Katika Biblia.

2. Biblia ni nini?

   Jibu: Ni vitabu 66 vilivyovuviwa na Mungu ambavyo vinatufundisha kuhusu Mungu na jinsi tunavyoweza kuwa watakatifu kama yeye alivyo mtakatifu

3. Nani aliandika Biblia?

   Jibu: Watu zaidi ya 40 waliongozwa na kuvuviwa na Mungu kupitia kipindi cha zaidi ya miaka 1,600.

4. Taja majina ya vitabu vitano katika Biblia vinavyoitwa Sheria.

   Jibu: Mwanzo, Kutoka, Mambo Ya Walawi, Hesabu, Kumbukumbu La Torati

5. Ujumbe wa Sheria ni nini?

   Jibu: Mungu ni mtakatifu, na anataka sisi tuwe kama yeye.

6. Taja majina ya vitabu vya historia katika Agano la Kale.

   Jibu: Yoshua, Waamuzi, Ruthu, 1 na 2 Samweli, 1 na 2 Wafalme, 1 na 2 Mambo Ya Nyakati, Ezra, Nehemia, Esta.

7. Ujumbe wa vitabu vya historia ni upi?

   Jibu: Mambo mazuri yanakuja tunapomfuata Mungu kwa moyo wote. Mambo mabaya yanakuja tusipomfuata.

8. Taja majina ya vitabu vya mashairi katika Agano la Kale.

   Jibu: Ayubu, Zaburi, Mithali, Mhubiri, Wimbo Ulio Bora.

9. Ujumbe wa vitabu vya mashairi ni upi?

   Jibu: Tunabarikiwa tunapomtafuta Mungu katika hali zote.

10. Taja majina ya vitabu vya manabii wakubwa katika Agano la Kale.

    Jibu: Isaya, Yeremia, Maombolezo, Ezekieli, Danieli.

11. Taja majina ya vitabu vya manabii wadogo katika Agano la Kale.

    Jibu: Hosea, Yoeli, Amosi, Obadia, Yona, Mika, Nahumu, Habakuki, Sefania, Hagai, Zekaria, Malaki.

12. Kwa nini hawa wanaitwa manabii “wadogo”?

    Jibu: Ni vitabu vifupi kuliko vya manabii wakubwa.

13. Ujumbe wa manabii ni upi?

    Jibu: Irudieni sheria na mpendeni Mungu.

14. Taja vitabu vya injili katika Agano Jipya.

    Jibu: Mathayo, Marko, Luka, Yohana.

15. Ujumbe wa vitabu vya injili ni upi?

    Jibu: Yesu alikuja, Akaishi, akafa, na alifufuka kwa ajili yetu.

16. Taja vitabu vinavyoelezea historia ya kanisa baada ya ufufuo wa Yesu.

    Jibu: Matendo Ya Mitume.

17. Ujumbe wa Matendo ya Mitume ni upi?

    Jibu: Roho Mtakatifu alikuja kanisani, na Neno la Mungu likaenea.

18. Taja nyaraka za Paulo.

    Jibu: Warumi, 1 na 2 Wakorintho, Wagalatia, Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, 1 na 2 Wathesalonike, 1 na 2 Timotheo, Tito, Filemoni.

19. Ujumbe wa nyaraka za Paulo ni upi?

    Jibu: Ishi katika neema ya Mungu na haki yake.

20. Taja nyaraka majina ya nyaraka za jumla.

    Jibu: Waebrania, Yakobo, 1 na 2 Petro, 1 na 2 na 3 Yohana, Yuda

21. Ujumbe wa nyaraka za jumla ni upi?

    Jibu: Jinsi ya kuishi duniani kama watu wa Mungu.

22. Taja jina la kitabu cha mwisho katika Biblia.

    Jibu: Ufunuo.

23. Ujumbe wa Ufunuo ni upi?

    Jibu: Yesu ni Mfalme wa wafalme na anakuja upesi kwa ajili ya kanisa lake la ushindi.

24. Taja vitabu vyote 66 vya Biblia

    Jibu:

    **Agano la Kale**

    Mwanzo, Kutoka, Mambo Ya Walawi, Hesabu, Kumbukumbu La Torati,
    Yoshua, Waamuzi, Ruthu, 1 na 2 Samweli, 1 na 2 Wafalme, 1 na 2 Mambo Ya Nyakati, Ezra, Nehemia, Esta,
    Ayubu, Zaburi, Mithali, Mhubiri, Wimbo Ulio Bora,
    Isaya, Yeremia, Maombolezo, Ezekieli, Danieli,
    Hosea, Yoeli, Amosi, Obadia, Yona, Mika, Nahumu,
    Habakuki, Sefania, Hagai, Zekaria, Malaki

    **Agano Jipya**

    Mathayo, Marko, Luka, Yohana, Matendo Ya Mitume, Warumi, 1 na 2 Wakorintho, Wagalatia, Waefeso, Wafilipi, Wakolosai,
    1 na 2 Wathesalonike, 1 na 2 Timotheo, Tito,
    Filemoni, Waebrania, Yakobo, 1 na 2 Petro,
    1 na 2 na 3 Yohana, Yuda, Ufunuo

25. Ujumbe wa vitabu hivi 66 vilivyovuviwa ni upi?

    Jibu: Vinatufundisha kuhusu Mungu na jinsi tunavyoweza kuwa watakatifu; jinsi tunavyoweza kukombolewa na kubadilishwa kuwa mfano wa Yesu Kristo.[1]

## Maswali kuhusu Amri Kumi

26. Amri za Mungu ni kitu gani?

    Jibu: Ni taswira ya Mungu alivyo na ahadi ya tunavyoweza kuwa.

27. Amri kumi zinapatikana wapi katika Biblia?

    Jibu: Katika Kutoka 20:1-17

28. Amri Kumi ni zipi?

    Jibu: Amri zilizotolewa kwa watu wa Mungu Mlima Sinai.

29. Nani alitoa Amri Kumi?

    Jibu: Mungu

30. Nani aliyepokea Amri Kumi?

    Jibu: Musa

[1] Kauli, “jinsi tunavyoweza kukombolewa na kubadilishwa kuwa mfano wa Yesu Kristo” “imeongezwa kwenye jibu la awali.

31. Amri ya kwanza inasema "Usiwe na miungu mingine ila mimi" Amri hii ina maanisha nini?

    Jibu: Daima tunapaswa kumweka Mungu wa kwanza.

32. Amri ya pili inasema: "Usijifanyie sanamu ya kuchonga..." Amri hii inamaanisha nini?

    Jibu: Ni kosa kuabudu kitu chochote isipokuwa Mungu.

33. Amri ya tatu inasema: "Usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako..." Amri hii inamaanisha nini?

    Jibu: Tunapaswa kulitaja jina la Mungu kwa heshima kubwa.

34. Amri ya nne inasema: "Ikumbuke siku ya Sabato uitakase..." Amri hii inamaanisha nini?

    Jibu: Tunapaswa kumwabudu Mungu Jumapili na kupumzika.

35. Amri ya tano inasema: "Waheshimu baba yako na mama yako..." Amri hii inamaanisha nini?

    Jibu: Tunapaswa kuwapenda na kuwatii wazazi wetu.

36. Amri ya sita inasema: "Usiue." Amri hii inamaanisha nini?

    Jibu: Hatupaswi kuua watu wengine bila sababu ya haki.

37. Amri ya saba inasema: "Usizini." Amri hii inamaanisha nini?

    Jibu: Ngono inapaswa kuwa ndani ya ndoa tu.

38. Amri ya nane inasema: "Usiibe." Amri hii inamaanisha nini?

    Jibu: Hatupaswi kuchukua vitu visivyo vyetu.

39. Amri ya tisa inasema: "Usimshuhudie jirani yako uongo." Amri hii inamaanisha nini?

    Jibu: Tunapaswa kusema ukweli siku zote.

40. Amri ya kumi inasema: "Usitamani..." Amri hii inamaanisha nini?

    Jibu: Tunapaswa kuridhika na vitu ambavyo Mungu ametupa.

41. Yesu alisema ni amri gani mbili kuu?

    Jibu: Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote; na mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.

42. Kwa nini amri hizi zote ni muhimu kwetu?

    Jibu: Zinatuonyesha maisha ambayo Mungu Mtakatifu anayatamani kwetu.

Swali la Ziada: Taja maandiko kamili ya Amri Kumi kama yalivyotolewa katika Kutoka 20:1–17.

## Maswali kuhusu Sala ya Bwana

43. Nani aliyesali Sala ya Bwana kwa mara ya kwanza?

    Jibu: Yesu, alipowafundisha wanafunzi wake kumi na wawili jinsi ya kusali.

44. Sala ya Bwana inapatikana wapi katika Biblia?

    Jibu: Katika Mathayo 6:9-13

45. Maneno ya Sala ya Bwana ni yapi?

    Jibu:

    Baba yetu uliye mbinguni,
    Jina lako litukuzwe,
    Ufalme wako uje,
    Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.
    Utupe leo riziki yetu.
    Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tusamehevyo wadeni wetu.
    Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.
    Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

46. Maana ya “Jina lako litukuzwe” ni nini?

    Jibu: Tunataka kumheshimu na kumpenda Mungu wetu Mtakatifu.

47. Maana ya “Ufalme wako uje” ni nini?

    Jibu: Mungu ni Mfalme wetu. Tunataka watu wote duniani wamjue kama Mfalme.

48. Maana ya “Mapenzi yako yatimizwe hapa, duniani kama huko mbinguni” ni nini?

    Jibu: Tunataka kila kitu ambacho Mungu anataka kitendeke.

49. Maana ya “Utupe leo riziki yetu” ni nini?

    Jibu: Tunaomba Mungu atupatie mahitaji yetu yote.

50. Maana ya “Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tusamehevyo wadeni wetu” ni nini?

    Jibu: Tunaomba Mungu atusamehe kama tunavyowasamehe wengine.

51. Maana ya “Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu” ni nini?

    Jibu: Tunaomba Mungu atulinde dhidi ya dhambi zote.

52. Maana ya "Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele" ni nini?

    Jibu: Mungu ni Mfalme Mwenye Nguvu zote anayetawala mbinguni na duniani milele.

53. Kwa nini Sala ya Bwana ni muhimu?

    Jibu: Inatusaidia kumtazama Mungu kama Baba yetu Mtakatifu.

## Maswali kuhusu Heri

54. Heri ni nini?

    Jibu: Mafundisho ya Yesu kuhusu tabia takatifu.

55. Heri zinapatikana wapi katika Biblia?

    Jibu: Katika Mathayo 5:3-10.

56. Taja Heri hizo.

    Jibu:

    Heri walio maskini wa roho;
    Maana ufalme wa mbinguni ni wao.

    Heri wenye huzuni;
    Maana hao watafarijika.

    Heri wenye upole,
    Maana hao watairithi nchi.

    Heri wenye njaa na kiu ya haki;
    Maana hao watashibishwa.

    Heri wenye rehema;
    Maana hao watapata rehema.

    Heri wenye moyo safi;
    Maana hao watamwona Mungu.

    Heri wapatanishi;
    Maana hao wataitwa wana wa Mungu.

    Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki;
    Maana ufalme wa mbinguni ni wao.

57. Je, kuwa maskini wa roho kunamaanisha nini?

    Jibu: Kukubali kuwa umetenda dhambi na unahitaji msaada wa Mungu.

58. Je, kuwa na huzuni kunamaanisha nini?

Jibu: Kuhuzunika kwa mambo yanayomhuzunisha Mungu.

59. Je, kuwa mpole kunamaanisha nini?

Jibu: Kumkabidhi Mungu maisha yako ili ayaongoze.

60. Je, kuwa na njaa na kiu ya haki kunamaanisha nini?

Jibu: Kutamani kwa kweli viwango vya Mungu katika maisha yako.

61. Je, kuwa mwenye rehema kunamaanisha nini?

Jibu: Kuwa na huruma kwa watu wote.

62. Je, kuwa na moyo safi kunamaanisha nini?

Jibu: Kumpenda Mungu kwa moyo wako wote.

63. Je, kuwa mpatanishi kunamaanisha nini?

Jibu: Kusaidia watu kuwa marafiki wa Mungu na wao kwa wao.

64. Je, kuudhiwa kwa ajili ya haki kunamaanisha nini?

Jibu: Kukubali kuteseka kwa furaha kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

## Maswali Kuhusu Mungu

65. Mungu wako wangapi?

Jibu: Kuna Mungu mmoja tu.

66. Kuna nafsi ngapi katika huyo Mungu mmoja?

Jibu: Tatu—Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu.

67. Neno gani linaelezea Mungu vizuri zaidi?

Jibu: Mungu ni mtakatifu.

68. Mungu ana umri gani?

Jibu: Mungu ni wa milele. Alikuwepo daima na atakuwepo daima.

69. Mungu yuko wapi?

Jibu: Mungu yuko kila mahali anapotaka kuwa.

70. Mungu anaweza kufanya nini?

Jibu: Mungu anaweza kufanya chochote anachotaka kufanya.

71. Mungu anajua nini?

    Jibu: Mungu anajua kila kitu anachotaka kujua.

72. Je, kuna kitu chochote chenye nguvu zaidi kuliko Mungu?

    Jibu: Hapana.

73. Mungu ni Muumbaji. Aliumba nini?

    Jibu: Kila kitu.

74. Kwa nini Mungu alikuumba?

    Jibu: Ili apate kunipenda na kufurahia kuwa nami.

## Maswali Kuhusu Mwanadamu, Dhambi, na Wokovu

75. Wanaume na wanawake ni nani?

    Jibu: Ni watu wanaoweza kumjua na kumpenda Mungu.

76. Wazazi wetu wa kwanza walikuwa nani?

    Jibu: Adamu na Hawa.

77. Nini kilichowafanya Adamu na Hawa kuwa tofauti na wanyama wote?

    Jibu: Adamu na Hawa walikuwa na roho; wanyama hawana.

78. Je, una roho?

    Jibu: Ndiyo, nina roho ambayo haitakufa milele.

79. Dhambi ni nini?

    Jibu: Ni kutotii sheria ya Mungu unayoijua.

80. Dhambi hufanya nini?

    Jibu: Inaharibu uhusiano wa upendo kati yetu na Mungu.

81. Nani alitenda dhambi ya kwanza?

    Jibu: Adamu na Hawa.

82. Adamu na Hawa walikosea kwa kufanya nini?

    Jibu: Walikula tunda ambalo Mungu aliwakataza kula na wakavunja uhusiano naye.

83. Nani aliwajaribu Adamu na Hawa kutenda dhambi?

    Jibu: Ibilisi.

84. Dhambi yao iliathiri vipi maisha yetu?

Jibu: Adamu na Hawa walitupatia dhambi; sisi sote tunazaliwa tukiwa wenye dhambi.

85. Wenye dhambi wanastahili nini?

Jibu: Adhabu ya Mungu na mauti.

86. Je, tunaweza kwenda mbinguni tukiwa wenye dhambi kwa makusudi?

Jibu: Hapana.

87. Tukifa hatuendi mbinguni, basi tunaenda wapi?

Jibu: Kuzimu.

88. Wokovu ni nini?

Jibu: Kusamehewa dhambi zetu kwa imani katika kifo, maziko, na ufufuo wa Yesu, na kumpenda Mungu.

89. Kwa nini tunahitaji wokovu?

Jibu: Kwa sababu sisi sote ni wenye dhambi.

90. Ni nini kinachohitajika ili kuokolewa?

Jibu: Kwa neema tunaokolewa kwa imani katika Kristo Yesu.

91. Je, kuna njia nyingine ya kuokolewa?

Jibu: Hapana, tunaokolewa tu kwa neema kupitia imani katika Kristo Yesu.

92. Tunapookolewa kutoka dhambini, nini hutokea?

Jibu: Tunampenda Mungu na jirani, na tunakua katika kutamani kumpendeza.

## Maswali kumhusu Yesu

93. Yesu ni nani?

Jibu: Yesu ni Mungu aliyefanyika mwanadamu, Mwokozi wetu.

94. Mwokozi ni nani?

Jibu: Ni mwokozi pekee anayetuokoa kutoka katika dhambi zetu.

95. Yesu ni mwanadamu au Mungu?

Jibu: Yeye ni mwanadamu mkamilifu na Mungu mkamilifu pia.

96. Nini kilikuwa cha pekee kuhusu kuzaliwa kwa Yesu?

Jibu: Alizaliwa na Bikira Maria kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

97. Yesu alifanya nini alipokuwa akiishi karibu miaka 2,000 iliyopita?

Jibu: Aliwafundisha wanafunzi wake, aliwahurumia maskini, na alikufa msalabani kulipia dhambi zetu.

98. Kulipia dhambi zetu kunamaanisha nini?

Jibu: Kunamaanisha kwamba Yesu alichukua adhabu tuliyostahili kwa kufa msalabani ili tuweze kuwa na uhusiano na Mungu.

99. Nini kilitokea baada ya Yesu kufa?

Jibu: Baada ya kuwekwa kaburini

## Maswali kumhusu Roho Mtakatifu

100. Roho Mtakatifu ni nani?

Jibu: Yeye ni nafsi ya tatu ya Mungu wa Utatu.

101. Roho Mtakatifu alikuja lini kama Yesu alivyoahidi?

Jibu: Wakati wa sikukuu ya Kiyahudi ya Pentekoste, siku 50 baada ya kufufuka kwa Yesu.

102. Pentekoste ni nini?

Jibu: Ni siku ya kuzaliwa kwa kanisa, wakati Roho Mtakatifu alipowajaza waumini wa Yesu.

103. Roho Mtakatifu anafanya nini leo?

Jibu: Anawatakasa waumini.

104 Roho Mtakatifu anawatakasa watu kwa njia gani?

Jibu: Anawathibitishia na kuwasafisha kutoka dhambini, anawafundisha na kuwaongoza, anawapa nguvu ya kiroho, karama za kiroho, na tunda la Roho.

105. Tunda la Roho ni nini?

Jibu: Tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, fadhili, uaminifu, upole, na kiasi.

106. Karama ya Roho ni nini?

Jibu: Ni uwezo tunaopokea kutoka kwa Roho Mtakatifu wa kusaidia kutimiza agizo kuu.

107. Agizo Kuu ni nini?

Jibu: Ni maagizo ambayo Yesu aliwapa wanafunzi wake waende wakafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, wakiwabatiza na kuwafundisha kuyatii mafundisho yake.

108. Ushuhuda wa Roho ni nini?

Jibu: Ni kujua ndani ya moyo kuwa imani yetu inampendeza Mungu.

109. Roho Mtakatifu anaweza kunisaidiaje?

Jibu: Anaweza kunisaidia kumpenda Mungu na kutii mapenzi yake kwa moyo wote.

110. Kuwa Mkristo "mkamilifu" kunamaanisha nini? [2]

Jibu: Kunamaanisha kumpenda Mungu kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote.

## Maswali Kuhusu Mambo ya Mwisho

111. Je, Yesu atarudi tena kwa namna binafsi na inayoonekana?

Jibu: Ndiyo.

112. Kwa nini Yesu atarudi tena?

Jibu: Ili alipokee kanisa lake kwake.

113. Hili litafanyika lini?

Jibu: Hatujui ni lini, kwa hiyo tunapaswa kuwa tayari kila wakati.

114. Tunaweza kujiandaa vipi?

Jibu: Kwa kuishi katika uhusiano wa upendo na Mungu kila wakati.

115. Nini kitatokea baada ya Yesu kurudi tena?

Jibu: Watu wote watahukumiwa, na Shetani atashindwa kabisa.

116. Baada ya Shetani kushindwa, nini kitatokea?

Jibu: Tutampenda Mungu na kumfurahia milele.

[2] Swali hili lilikuwa Swali la 119 katika mwongozo wa awali.

**Vifungu vya Kukariri**

- Kutoka 19:3-6
- Kutoka 20:1-17 – Amri Kumi
- Kumbukumbu la Torati 6:4-9
- Zaburi 1
- Zaburi 23
- Zaburi 24
- Zaburi 121
- Zaburi 139
- Mathayo 7:21-27
- Mathayo 28:18-20
- Yohana 3:16-21
- 1 Wakorintho 12:1-13
- Wagalatia 5:16-25
- Waefeso 6:10-17
- Wafilipi 2:5-11
- Waebrania 12:1-3
- 1 Petro 2:9-12
- Ufunuo 21:4-8

# Kwa Wazazi: Zana ya 3

## Kusudi la Zana hii

Chombo hiki kinatoa kanuni za maisha kutoka katika kitabu cha Mithali kwa ajili ya matumizi katika familia, shule, au mazingira mengine ya kujifunzia. Nyenzo hii haijakusudiwa kufundishwa yote kwa mara moja kama somo moja kamili.
Ni bora kufundisha na kujadili kanuni moja au mbili kwa siku.

## Mbinu za Ufundishaji

(1) Mtu mmoja asome mistari ya Biblia inayohusiana na kanuni husika. Kama kuna mistari mingi, mzazi au mwalimu anaweza kuchagua ipi itumike.

(2) Mzazi au mwalimu ahakikishe kuwa wasikilizaji wanaelewa maneno na kauli zilizomo katika mistari hiyo.

(3) Kisha, mzazi au mwalimu anaweza kueleza kanuni inayotokana na andiko hilo.

(4) Mzazi au mwalimu na wengine wanaweza kueleza hali halisi za maisha ambapo kanuni hiyo inatumika.

## Dhana Muhimu Katika Kitabu cha Mithali

Kumcha Mungu ni dhana muhimu sana katika kitabu cha Mithali. Kumcha Mungu kwa usahihi kunamaanisha kujua mambo matatu: kumjua Mungu alivyo, kuelewa kuwa tunapaswa kumtii, na kutambua kuwa tutahukumiwa kwa kutotii.

Hekima ni mada kuu katika Mithali. Kuwa na hekima ni kukubali na kufuata mtazamo na maadili ya Mungu. Mungu huona mambo kama yalivyo kweli, kwa hiyo tunakuwa na hekima tunapoamini kile Mungu anasema na kufuata maagizo yake.

Wazazi na walimu wanapaswa kujitoa binafsi kufuata kanuni kutoka katika kitabu cha Mithali. Wanapaswa kuonyesha kwa vitendo utii wa kanuni hizo katika maisha yao. Pia wanapaswa kuzifundisha kanuni hizo kwa watoto wao na wanafunzi, na kutafuta njia za kuzitumia katika hali halisi za maisha.

# Zana ya 3
# Kanuni kutoka Mithali

1. Kujifunza hekima ya Mungu ni jambo la muhimu zaidi ninaloweza kufanya (Mithali 2:4-5, Mithali 4:5).
2. Sipaswi kuamini kila kitu ninachosikia (Mithali 14:15).
3. Napaswa kumfuata Mungu katika maamuzi yangu yote ili aniongoze (Mithali 3:5-6).
4. Napaswa kusikiliza ushauri na hekima kutoka kwa baba na mama yangu (Mithali 1:8).
5. Ushauri mwema huleta baraka maishani mwangu na hunifanya niwe msaada kwa wengine (Mithali 10:17).
6. Nikikataa mafundisho mazuri, nitakumbana na maangamizi (Mithali 13:18).
7. Mafundisho mazuri hunisaidia kukua na kuimarika (Mithali 9:9).
8. Mungu hataki niwe mkatili au mdanganyifu (Mithali 3:31-32).
9. Ninahitaji kuwa na nia sahihi moyoni mwangu (Mithali 4:23, Mithali 12:5).
10. Mungu anajua sababu ya kweli ya kile ninachofanya (Mithali 16:2).
11. Mimi ni mpumbavu nikikataa maarifa na kurekebishwa (Mithali 1:22, Mithali 12:1).
12. Kumfuata Mungu kunanilinda dhidi ya maangamizi mengi (Mithali 1:33).
13. Ninaweza kuishi bila hofu kwa kumtumaini Mungu (Mithali 3:25-26).
14. Lazima nimtumaini Mungu badala ya kutegemea ufahamu na uwezo wangu mwenyewe (Mithali 3:7, Mithali 11:2, Mithali 12:15).
15. Siwezi kuficha dhambi milele (Mithali 10:9).
16. Sheria za Mungu hunilinda na kunisaidia (Mithali 6:23-24).
17. Mimi ni mwenye nguvu ikiwa ninaweza kujizuia na kudhibiti hisia zangu (Mithali 16:32, Mithali 25:28).
18. Nikizungumza bila kufikiria, naweza kuumiza wengine na mimi mwenyewe (Mithali 10:8, Mithali 10:21).
19. Napaswa kuepuka watu wanaonishawishi kufanya mabaya (Mithali 1:10-15, Mithali 4:14-15, Mithali 14:7, 16).
20. Napaswa kuchagua rafiki mwenye tabia ninayopenda kuwa nayo (Mithali 13:20).

21. Mungu anaona kila kitu ninachofanya (Mithali 5:21, Mithali 15:3).
22. Rafiki zangu watanithamini ikiwa nitakuwa mwaminifu na mwenye kutegemewa (Mithali 19:22).
23. Kushiriki maisha na wapendwa ni bora kuliko anasa (Mithali 15:17).
24. Napaswa kutenga muda wa kutosha kabla ya kufanya maamuzi (Mithali 21:5, Mithali 19:2).
25. Ikiwa nina hekima, nitapenda maarifa na kuwa mwangalifu (Mithali 8:12).
26. Nitakataa pombe kwa kuwa huleta tabia mbaya (Mithali 20:1).
27. Sipaswi kulipiza kisasi bali kumtumaini Mungu aniletee haki (Mithali 20:22).
28. Napaswa kutafuta amani badala ya ugomvi (Mithali 3:30, Mithali 20:3, Mithali 10:12).
29. Sipaswi kusema uongo ili kuwadhuru wengine (Mithali 30:10).
30. Ikiwa ninaaminika, sitasambaza siri ili kusababisha madhara (Mithali 11:13, Mithali 20:19).
31. Tabia njema hunifanya niseme ukweli (Mithali 13:5, Mithali 14:5).
32. Napaswa kufikiri kwa makini kabla ya kuzungumza (Mithali 15:28).
33. Sipaswi kuwa na haraka ya kukosoa au kugombana (Mithali 11:12, Mithali 17:27).
34. Mimi ni mpumbavu nikikasirika haraka (Mithali 12:16, Mithali 14:29).
35. Napaswa kuwa mwangalifu ili Maneno yangu kuleta baraka kwa watu, si madhara (Mithali 12:18, Mithali 12:25, Mithali 16:24, Mithali 18:21).
36. Napaswa kusema ukweli kila wakati (Mithali 4:24, Mithali 12:17).
37. Napaswa kusikiliza ukweli wote kabla ya kutoa maoni (Mithali 18:13).
38. Nikizungumza kupita kiasi, nitasema maneno ya dhambi (Mithali 10:19).
39. Napaswa kuwaheshimu wazee kwa namna ya pekee (Mithali 16:31, Mithali 20:29).
40. Wema na ukweli huniletea baraka za Mungu na heshima kutoka kwa watu (Mithali 3:3-4).
41. Mungu hunirudi ninapokosea kwa sababu ananipenda (Mithali 3:12).
42. Kabla ya kufanya uamuzi, napaswa kufikiria matokeo (Mithali 22:3).
43. Nikitenda dhambi, nitakumbana na matokeo mabaya (Mithali 6:27).
44. Nikikuwa mvivu, nitaishi kwa shida kama vile nimeporwa (Mithali 6:10-11, Mithali 19:15).

45. Sipaswi kuwa mvivu kwa sababu uvivu ni sawa na uharibifu (Mithali 18:9).

46. Napaswa kufanya kazi na kutumia fursa ili kuboresha maisha yangu ya baadaye (Mithali 6:6-8, Mithali 20:13).

47. Sipaswi kuwa mkatili kwa wanyama (Mithali 12:10).

48. Matendo yangu hujenga sifa yangu (Mithali 20:11).

49. Napaswa kujipanga kustahimili wakati wa shida (Mithali 24:10).

50. Napaswa kufanya kazi kwa wakati ufaao ili nipate matokeo bora (Mithali 10:5, Mithali 20:4).

51. Uvivu huleta matatizo, lakini kazi hufungua milango ya fursa (Mithali 15:19, Mithali 14:23).

52. Sipaswi kutafuta faida kwa njia za udanganyifu (Mithali 10:2, Mithali 11:18, Mithali 15:27).

53. Naweza kupata pesa kwa kufanya kazi na kujiwekea akiba (Mithali 10:4, Mithali 12:11, Mithali 13:11, Mithali 21:20, Mithali 28:19).

54. Mungu atanipatia mahitaji yangu ikiwa nitakuwa mwenye haki (Mithali 10:3).

55. Mungu atabariki mali na fedha zangu nikimtolea (Mithali 3:9-10).

56. Napaswa kuwalipa watu wanaonidai kwa haraka iwezekanavyo (Mithali 3:27).

57. Napaswa kuwa mkarimu kwa wenye uhitaji (Mithali 11:24-25, Mithali 14:21, Mithali 19:17, Mithali 21:13).

58. Pesa hazinilindi, bali haki ndiyo inayonilinda (Mithali 2:7-8, Mithali 10:9, Mithali 10:25, Mithali 11:28).

59. Sipaswi kuchukua jukumu la madeni ya mtu mwingine (Mithali 6:1-3, Mithali 17:18).